WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKINOLOJIA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

Shule ya Sekondari Igombavanu,

S.L.P.461,

Mafinga.

Kumb.Namb: IGSS/F1/VOL-1/ 2021/01 **Tarehe: 09/12/2020.**

NAMBA ZA SIMU: MKUU WA SHULE : 0763961637

MAKAMU : 0757019049

Kwa MZAZI/MLEZI WA : _____

Kijiji cha: _____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IGOMBAVAVU WILAYA YA MUFINDI MKOA WA IRINGA MWAKA 2021.

Awali ya yote ninachukua fursa hii kukupongeza kwa kufaulu mtihani wako wa darasa la saba,kitendo ambacho kimekuwezesha kuchaguliwa kujiunga na shule yetu kuanza kidato cha kwanza mwaka 2021

Ni matumaini yangu kuwa bahati hii utaitumia vizuri ili uweze kutumia juhudi na maarifa ya hali ya juu kukuwezesha kufanikiwa katika masomo na shughuli nyingine hapa shuleni kama vile Uzalishaji mali, michezo n.k. Aidha ni mategemeo ya walimu wote hapa shuleni kuwa utakuwa na nidhamu nzuri na utaendelea na kufuata sheria na kanuni zote za shule pamoja na masharti yote ya kujiunga kama yalivyoorodheshwa hapa chini.

Shule ya sekondari Igombavanu ni ya KUTWA na ni ya MCHANGANYIKO.Masomo huanza saa 1:30 asubuhi na kuisha saa 8:30 mchana, baada ya chakula cha mchana wanafunzi wote hutakiwa kuingia darasani saa 10:00 alasiri hadi saa 12:00 jioni kwa masomo ya ziada. Shule hii ipo wilaya ya Mufindi,Kata ya Igombavanu,Kijiji cha Lugodalutali.Hali ya hewa ni ya baridi na ni nzuri kwa masomo.

SHULE ITAFUNGUA tarehe 11/01/2021, mwanafunzi unatakiwa kufika shuleni siku ya JUMATANO tarehe 06/01/2021 ukiwa na mzazi/mlezi wako kwa ajili ya kujiandikisha , unapokuja hakikisha una vitu vifuatavyo:-

1. fomu iliyojazwa na daktari na kugogwa mhuri 2. fomu ya ahadi ya mzazi/mlezi ikiwa imejazwa.
3. Namba ya simu

MASOMO yanayofundishwa katika shule hii ni Hisabati,Jiografia,Uraia,Elimu viumbe (Biolojia) ,Kiswahili ,Kiingereza,Fizikia,Kemia, na Historia.

Unapokuja shule uwe na vitu vifuatavyo; 1.daftari 10 za msomi kwa ajili ya mazoezi ya darasani **2.**Counter book 10 na tutazikagua kwa matumizi ya mwanafunzi **, 3.**peni na penseli za kuandikia, **4.**mkebe wenye vifaa vyote vya kujifunzia, **5.**Baadhi ya vitabu vya masomo kwa ajili ya mwanafunzi kufanya marudio **6**. Rimu ya karatasi kwa ajiri ya kufanyia majaribio na mitihani mbalimbali ya kila wiki

na kila mwezi **7**. UFAGIO WA CHELEWA (Hivi vyote itakuwa ni mali ya mwanafunzi na atawajibika kutunza mahali salama**)** .Pia **uje na KOPI YA CHETI CHA KUZALIWA CHA MWANAFUNZI HUYU**.

SARE YA SHULE WASICHANA	**NA**	**SARE YA WAVULANA**
1.wasichana ni sketi 1kijani na 1 nyeusi.		1 .wavulana ni suruali 1kijani na 1nyeusi.
2.Blauzi 2 nyeupe tetroni mikono mirefu.		2 .shati 2 nyeupe tetroni mikono mirefu.
3.Viatu vya ngozi jozi 2 vyeusi na sio buti.		3 Viatu vya ngozi jozi 2 vyeusi na sio buti.
4 Soksi jozi 2 nyeupe		4 soksi jozi 2 nyeusi
5 Tai nyeusi 1 na kijani 1.		5 Tai nyeusi 1 na kijani 1.
6.Sweta 1 rangi ya light blue.		6.Sweta 1 rangi ya light blue.
7.Viatu vya michezo(raba jozi 1)		7.Viatu vya michezo(raba/njumu jozi 1)
8.T-shirt 1 njano		8.T-shirt 1 njano
9.Nywele fupi.		9.Nywele fupi.
10.Hijabu kwa msichana wa kiisilamu.		

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Binadamu asilani,kukaa pamoja si bure wana malengo.Aidha Taasisi ya Elimu kama hii yetu pia ina malengo,Shule zinaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya Mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na.10 ya Mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, kufikia malengo hayo lazima kuwe na kanuni na taratibu maalum za kufuatwa.Hususani mwanafunzi wa Igombavanu sekondari anapaswa kufuata na kutekeleza kanuni na taratibu zifuatazo;

a)Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na kwa jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
b)Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;

c)Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(preparation) kwani shule ina umeme;
d)Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
e)Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
f)Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule;

g)Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
h)Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
i)Kutunza na kuhifadhi mahali salama mali za umma.

Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa Shule;

a)Wizi.

b)Uasherati na Ushoga;

c)Ubakaji;

d)Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kubeli na kadhalika.

e)Kupigana au kupiga;

f)Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

g)Kudharau bendera ya Taifa.

h)Kuwa mjamzito au kupata mimba.

i)Kuoa au kuolewa.

j)Kutoa mimba.

k)Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

l)Kukataa adhabu kwa makusudi.

m)**Kuwa na simu ya mkononi**.

n) Mwanafunzi Kutohudhuria shule kwa makusudi siku 90 mfululizo.

o) Utoro sugu

NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA

KARIBU SANA IGOMBAVANU SEKONDARI

MKUU WA SHULE

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

SHULE YA SEKONDARI IGOMBAVANU

FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA MASHARTI YA KUPOKELEWA SHULENI

Kijiji cha _____

S.l.p_____Mafinga.

Tarehe_____

Mkuu wa shule,

Shule ya sekondari Igombavanu,

S.l.p 461, Mafinga.

YAH:KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IGOMBAVANU MWAKA 2020

A:MWANAFUNZI/MTOTO

Mimi……nimezaliwa …../……/……..;katika wilaya ya…….. nimesoma kwa makini barua ya maagizo ya kujiunga na shule yako pia sheria za shule.Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa Ninaikubali/Ninaikataa nafasi hiyo kwasababu…….....

Pia Nayakubali/Nayakataa masharti/Sheria za shule yako.

Saini ya mwanafunzi……. Tarehe……

B:MZAZI/MLEZI

Mimi……mzazi/mlezi wa…….Ambaye amechaguliwa kujiunga na shule yako,nimesoma maagizo ya kujiunga na shule na sheria zake. Ninaikubali/Ninaikataa nafasi hiyo (kwa anayekubali)Naahidi kumtimizia mtoto wangu maagizo yote ya kujiunga na shule katika muda uliopangwa.Pia nitashirikiana na shule yako daima katika kumkuza na kumlea mtoto wangu.Naahidi pia kusimamia nidhamu na maendeleo yake ya kitaaluma muda wote awapo shuleni . Mtoto wangu akipata wastani chini ya **45** nitawajibika kufika shuleni. Ahsante.

Jina la mzazi/mlezi……S.l.p……

Simu za mzazi/mlezi ni……/……/……

Simu za ndugu wa jirani ni ……..au……..au……

Tarehe…… Saini ya mzazi/mlezi……..

Δ Futa lisilohusika.Pia mzazi/mlezi ukibadili anuani,namba ya simu au ukihama tujulishe mara moja.

IGOMBAVANU SECONDARY SCHOOL P.O.BOX 461 MAFINGA.FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.

This form is to be completed / filled by Medical officer from any Tanzanian Government Hospital

1 .Student`s full name……..

2 .Age…….years

3 .Sex……

4 .Blood count (Red and White)…….

5 .Stool Examination…….

6 .Urine analysis…….

7 .Syphilis test…….

8. T.B test……

9. Eye test……

10 .Ears……..

11 .Chest……

12 .Spleen……

13 .Abdomen…….

14 .Pregnancy test……..

15 ……

ADDITIONAL INFORMATION e.g. Physical or chronicle of family diseases.etc

……

I certify that the above student is Fit/Unfit to pursue studies.

Full name:…… Signature……..

Designation…….. Section……Date……

STUDENT: You must bring this complete form when you come to school. No student may enroll without certificate of physical fitness.

THE HEADMASTER IGOMBAVANU SECONDARY SCHOOL